



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

OFISI YA HAKIMILIKI TANZANIA

**COSOTA**  
OFISI YA HAKIMILIKI TANZANIA

## TANGAZO

**TANGAZO LA KUKARIBISHA MAOMBI YA LESENI KWA KAMPUNI ZA UKUSANYAJI NA UGAWAJI WA MIRABAHA (COLLECTIVE MANAGEMENT ORGANIZATIONS – CMOs) TANZANIA BARA KATIKA DARAJA LA KAZI ZA FILAMU, KAZI ZA MUZIKI, KAZI ZA MAANDISHI, SANAA ZA MAONESHU NA UFUNDI.**

Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya mwaka 1999 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2022 kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2022 iliruhusu uanzishwaji wa Makampuni binafsi yatakayokuwa na jukumu la kukusanya na kugawa Mirabaha kwa pamoja yaani *Collective Management Organizations* (CMOs).

Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) inapenda kukaribisha Kampuni yoyote yenye nia ya kupatiwa Leseni ili kufanya kazi kama CMO Tanzania Bara katika daraja la Kazi za Filamu /kazi za Muziki/Kazi za Maandishi Sanaa za Maonesho au Sanaa za Ufundi kuwasilisha maombi rasmi kwa kuzingatia vigezo vinavyopatikana katika Kanuni za Hakimiliki na Hakishiriki (Kampuni za Ukusanyaji na Ugawaji wa Mirabaha) 2023, Toleo Namba 215 na 211 la tarehe 24 Machi, 2023. Kanuni hizi pia zinapatikana katika tovuti ya Ofisi: [www.cosota.go.tz](http://www.cosota.go.tz)

### **Masharti ya kupatiwa leseni kwa kampuni ni kama ifuatavyo;**

1. Iwe inamilikiwa na Watanzania (iwasilishe vitambulisho vya wamiliki wa Kampuni – Mf. Kitambulisho Taifa (NIDA), Pasi ya kusafiria)
2. Nakala za picha za wamiliki (passport size)
3. Iwe na Hati ya namba ya mlipakodi (TIN) kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)
4. Iwe na hati ya mlipa kodi (Tax clearance certificate) kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)
5. Iwe na Leseni ya biashara kutoka Mamlaka husika
6. Iwe na cheti ya usajili wa Kampuni kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)
7. Iwe na Hati ya usajili wa makampuni (Certificate of incorporation)
8. Iwe na *Memorandum and Article of Association*
9. Iwe na wasifu wa wamiliki
10. Taarifa za Kifedha za kibenki zilizothibitishwa (Current Certified Bank Statement)
11. Iwasilishe dhamana (security/Collateral) yenye thamani isiyopungua kiasi cha shilingi za Kitanzania milioni mia mbili Hamsini (Tsh. 250,000,000) kwa madaraja ya muziki na filamu na isiyopungua milioni hamshini (Tsh. 50,000,000) kwa madaraja ya Kazi za maandishi, kazi za sanaa za ufundi na maonesho.
12. Iwasilishe mpango kazi wa namna ambavyo Kampuni itakusanya na kugawa mirabaha kwa ufanisi.
13. Iwasilishe orodha ya uthibitisho wa Wanachama wasiopungua thelathini ambao inatarajia kuwawakilisha (majina, namba za simu na saina zao)
14. Iwe haijawahi kushtakiwa kwa makosa yoyote au kutiwa hatiani kwa makosa yoyote
15. Kufuata Sheria na kanuni zote za Nchi. (Namba 14 - Kampuni iwasilishe kiapo kutoka kwa Mwanasheria)

**Tafadhali tambua kuwa:** Maombi ya Leseni yatapokelewa ndani ya siku 30 kuanzia tarehe ya Tangazo hili na yawasilishwe kupitia anuani ifuatayo:

Katibu,  
Bodi ya Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA),  
S.L. P 6388,

**Dar es Salaam.**

Tafadhali andika neno “CMO” juu ya bahasha.

**Imetolewa na;**

Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA),  
S.L.P 6388, **Dar es salaam. SIMU: 0738 015013**  
**07 Machi, 2025**